

# TUSAIDIE KUELEWA ZAIDI KUHUSU WATU WAZIMA NA WATOTO WALIO NA UGONJWA WA ANEMIA SELIMUNDU



Asante kwa kuwa sehemu ya Pacific Sickle Cell Regional Collaborative (PSCRC) Minimum Data Set! Lengo letu lilikuwa kuelewa zaidi kuhusu watu wazima na watoto walio na ugonjwa wa anemia selimundu katika majimbo saba ya Pacific Redion. Data ilikusanywa kwenye maeneo yote kumi ya kimatibabu ya washiriki 407 kutoka Alaska, Arizona, California, Idaho, Nevada, Oregon na Washington kuanzia Mei 2016 hadi Agosti 2017.

## NINI?

Tuliwauliza watu wazima walio na ugonjwa wa anemia selimundu (miaka 18 na zaidi) na wazazi wa watoto walio na ugonjwa wa anemia selimundu kuhusu hali za hydroxyurea na kuhusu matatizo yoyote ambayo wanaweza kuwa nayo kutokana na dawa hiyo. Hydroxyurea ni dawa inayoweza kuwasaidia watoto na watu wazima walio na ugonjwa wa anemia selimundu kwa kupunguza matukio ya maumivu, siku kwenye hospitali na matukio ya dalili ya maumivu makali kwenye kifua.

## NANI?

Watu wazima 169 walio na ugonjwa wa anemia selimundu na wazazi 238 wa watoto walio na ugonjwa wa anemia selimundu. Nusu walikuwa wanaume na nusu wanawake. **Asilimia 93** walikuwa Waafrika Wamarekani na **asilimia 74** walitambuliwa kuwa na ugonjwa wa SS.



## HATUA ZINAZOFUATA:

PSCRC imefungua maeneo mengine hadi majimbo 13 ya

Magharibi. Watoa huduma wa PSCRC wanashirikiana ili kutambua njia bora za kuwasaidia watu wazima walio na ugonjwa wa anemia selimundu na wazazi wa watoto walio na ugonjwa wa anemia selimundu kuhusu dawa ya hydroxyurea ili uelewe kikamilifu manufaa ya dawa na hatari zozote. Tunafahamu kuwa dawa ya hydroxyurea ni salama unaposhirikiana kwa karibu na mtoa huduma wako wa afya. Daktari au muuguzi wako atakupua maagizo kuhusu kufanyiwa vipimo vya damu, kuhusu mara ambazo unakuja kwenye kliniki na kuhusu dozi sahihi kwako au mtoto wako.

## UNAWEZA KUFANYA NINI:

Zungumza na daktari au muuguzi wako ikiwa una swali lolote kuhusu ikiwa dawa ya hydroxyurea ni nzuri au si nzuri kwako. Ikiwa uliagizwa kutumia hydroxyurea lakini una tatizo au vikwazo vyovyote vya kuimeza, mfahamishe daktari au muuguzi wako. Unaweza kuunda mpango pamoja na mtoa huduma wako wa afya utakaoboresha afya yako!

Ilisasishwa Septemba 2020. **Kwa maelezo zaidi, tembelea: [pacificscd.org](http://pacificscd.org) au [casicklecell.org](http://casicklecell.org)**

## Asilimia 47 ya watu wazima na Asilimia 67 ya watoto walikuwa wakitumia hydroxyurea

**Watu wazima** walikuwa wamesema kuwa walikuwa na vizuizi vya kumeza hydroxyurea mara nyingi, ikilinganishwa na wazazi wa watoto (**asilimia 81** ya watu wazima walisema walikuwa na angalau kikwazo kimoja ikilinganishwa na **asilimia 57** ya wazazi)

**Watu wazima** walikuwa na wasiwasi kuhusu madhara ya matumizi ya dawa mara nyingi (**asilimia 22** ikilinganishwa na **asilimia 13** ya wazazi)

**Watu wazima** walisema kuwa kusahau kumeza dawa kulitokea mara nyingi (**asilimia 20** ikilinganishwa na **asilimia 8** ya wazazi)

